LONDA

KENYA HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE

RIPOTI YA 2020

PARADIGM INITIATIVE

www.paradigmhq.org

@ParadigmHQ

LONDA

KENYA HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI 2020 RIPOTI

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE

Imechapishwa na Paradigm Initiative
374 Borno Way, Yaba, Lagos, Nigeria
Email: media@paradigmhq.org
www.paradigmhq.org

Iliyochapishwa mnamo Aprili 2021

Ripoti iliyotolewa na Ekai Nabenyo
Timu ya Uhariri: 'Gbenga Sesan, Kathleen Ndongmo, Koliwe Majama, Margaret Nyambura Ndung'u, Mawaki Chango, Nnenna Paul-Ugochukwu and Thobekile Matimbe.
Ubunifu na Luce Concepts

This publication may be reproduced for non-commercial use in any form provided due credit is given to the publishers, and the work is presented without any distortion.

Copyright © 2021 Paradigm Initiative

Creative Commons Attribution 4.0 International (CC BY 4.0)

LONDA

KENYA HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI 2020 RIPOTI

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE

Asasi za kiraia zinaendelea kufanya kazi ili kuendeleza haki za dijitali na ujumuishi barani Afrika, kuhakikisha njia bora zinapitishwa katika sera na sheria. Ripoti hii inachambua hali ya haki za dijitali na ujumuishi nchini Kenya, ikichunguza ukiukaji na mapungufu, ikiangazia utumiaji na utekelezwaji wa sera na sheria, ikiangazia hatua muhimu na kutoa mapendekezo kwa mandhari ya dijitali nchini Kenya. Pamoja na ripoti kutoka nchi 20, toleo hili linaangazia kati ya maswala mengine, pengo la kidijitali lililozidishwa na janga la COVID-19 na kufichua ukiukaji kwenye nyanja tofauti kama vile faragha, ufikiaji wa habari, na uhuru wa kujieleza na msingi wa sheria na sera ulioelezewa vizuri.

PARADIGM INITIATIVE

@ParadigmHQ

YALIYOMO

UTANGULIZI 1

ATHARI ZA COVID-19 KWA HAKI ZA KIDIJITALI NA UJUMUISHI 1

FARAGHA, VITAMBULISHO VYA KIDIJITALI NA UFUATILIAJI 2

MATAMSHI YA CHUKI, TAARIFA POTOFU NA SHERIA ZA MAKOSA YA JINAI 3

KUTENGWA KIDIJITALI 4

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 4

UTAFITI MAALUM 5



Kenya ni kitovu cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kinachojulikana kwa jina lisilo rasmi kama 'Silicon Savannah' kwa ubunifu wake katika teknolojia. Hiyo haimaanishi kwamba Kenya haina changamoto zinazotokana na pengo la kidijatali.

UTANGULIZI

HAKI ZA DIJITALI NA UJUMUISHAI YA NCHI YA KENYA

Gharama ya ufikiaji wa mtandao ni mojawapo wa zile ghali zaidi katika eneo hili, hali ambayo imesababisha kutengwa kidijitali kwa vijana na wanawake. Hali hii imesababisha ukiukaji wa haki za binadamu kama vile haki ya kupata habari.

Nchi hii ni makazi ya mamia ya makampuni ya teknolojia na vile vile kampuni changa za TEHAMA. Hali ya wigo wa kidijitali nchini Kenya inaangaziwa katika sehemu hii ya ripoti. Takwimu katika sehemu hii zilipatikana kupitia mapitio ya ripoti anuwai za mamlaka za TEHAMA nchini, ripoti binafsi za kampuni na ripoti za kuaminika za vyombo vya habari.

ATHARI ZA COVID-19 KWA HAKI ZA KIDIJITALI NA UJUMUISHI

Janga la COVID-19 limefanya swala la ukosefu wa usawa katika ufikiaji mtandao na teknolojia za kidijitali nchini Kenya kujitokeza. Janga hili ambalo halikutarajiwa limekuwa thibitisho tosha la ukosekanaji wa usawa katika ufikiaji mtandao na teknolojia za kidijitali miongoni mwa vijana nchini Kenya. Ufurahiaji wa uhuru wa kujieleza mtandaoni mnamo 2020 nchini ulisababisha ongezeko la idadi ya watumiaji mtandao kwa sababu serikali haikuzuia ufikiaji.

Uhuru wa

kujieleza mtandaoni mnamo

Hadi kufikia 2020, Kenya ilikuwa na upenyaji wa mtandao wa takriban 87%. Kiwango hiki cha juu ni kwa sababu Kenya ni mwenyeji wa M-PESA, huduma ya pesa ya kutumia simu ya mkononi, na mfumo huu salama wa malipo unahimiza ufikiaji mtandao.[1] Kulingana na Mamlaka ya Mawasiliano nchini, usajili wa huduma za mtandao uliongezeka hadi kiwango cha 5.1% kati ya Aprili na Juni 2020 pale ongezeko la huduma lilipoongezeka kufuatia hatua za kukaa nyumbani zilizowekwa na serikali kufuatia kuchipuka kwa janga la COVID-19. Usajili uliongezeka hadi wasajili milioni 40.9 mnamo Juni 2020, kutoka milioni 38.9 katika kipindi kilichoishia Machi 2020. Mamlaka ya Mawasiliano nchini ilihusisha hali hii na ongezeko la hitaji la ufikiaji taarifa mtandaoni, ikiwemo pamoja na uhamishiaji wa huduma zaidi kwenye nyuga za kidijitali wakati wa kipindi cha janga.[2]

Vile vile, Kenya ina mfumo wa mahakama ulio na uhuru kwa kiasi kikubwa na umeendeleza sheria katika nyanja ya haki za kidijitali. Mahakama za sheria zimefanya maamuzi yanayoegemea katika kuhahikisha kuwa haki za kidijitali za wananchi zinaheshimiwa, faragha yao inahakikishiwa na kwamba raia wana uwezo wa kufikia mahakama kupata hako iwapo kuna madai ya ukiukwaji, kulingana na Muswada wa Haki wa nchi. Kwa kuongezea, Kenya ina Muswada imara na Kifungu cha 35 haswa kinatoa hakikisho kwa ufikiaji wa habari. Sheria ya Ufikiaji wa Habari ya 2016, inalenga kuwezeshesha kipengele hiki Kikatiba. Kuzidisha, Sheria ya Ulindaji Data inalenga kulinda data. Licha ya changamoto zilizowasilishwa na janga la COVID-19 ambazo zilielekeza tena umakini wa nchi, Kenya ilipiga hatua chanya katika haki za kidijitali na ujumuishaji wa kidijitali mnamo mwaka wa 2020. Baadhi ya maendeleo muhimu ni pamoja na yafuatayo.

FARAGHA, VITAMBULISHO VYA KIDIJITALI NA UFUATILIAJI

- **Kuteuliwa kwa Kamishna wa Data za Umma**

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 24 cha 2019 cha Ulindaji Data, Rais Uhuru Kenyatta alimteua Immaculate Kassait kama Kamishna wa Data za Umma nchini.[3] Kamishna anatarajiwa kuweka miundo na mifumo ya ulindaji wa data za Umma kulingana na maagizo yaliyotolewa na Mahakama Kuu katika kesi ya Nambari ya Huduma. Nambari ya Huduma ambayo ilizinduliwa mwanzoni mwa Desemba 2020 iliwasilisha changamoto zinazohusiana na ulindaji wa data na faragha.

Kamishna wa Data za Umma ana jukumu la kuanzisha na kudumisha sajili (rejista) ya wasimamizi wa data na wachakataji data; kutekeleza uangalizi kuhusu shughuli za uchakataji data na kupokea na kuchunguza malalamiko yoyote na mtu yeyote yanayohusiana na ukiukwaji wa haki chini ya Sheria. Sheria, kwa mfano, inahitaji kwamba data ya kibinafsi inaweza tu "kukusanywa kwa madhumuni wazi, maalum na halali na isifanyiwe kazi zaidi kwa njia ambayo haiendani na malengo hayo."[4]

1. See Share of internet users in Africa as of March 2020, by country, https://www.statista.com/statistics/1124283/internet-penetration-in-africa-by-country/
2. Fourth Quarter Sector Statistics Report for the Financial Year 2019/20 (April-June 2020), https://ca.go.ke/wp-content/uploads/2020/10/Sector-Statistics-Report-Q4-2019-2020.pdf
3. Immaculate Kassait sworn in as Data Commissioner, https://www.kbc.co.ke/immaculate-kassait-sworn-in-as-data-commissioner/
4. Data Protection Act, 2019 Available at http://kenyalaw.org/kl/fileadmin/pdfdownloads/Acts/2019/TheDataProtectionAct__No24of2019.pdf

KESI YA NAMBARI YA HUDUMA/ MFUMO WA KITAIFA WA UTAMBULISHO WA KIELEKTRONIKI (NIIMS)

Serikali ya Kenya ilianzisha hifadhi data ya kitaifa – mfumo wa Kitaifa wa Utambulisho wa Kielektroniki (NIIMS). Mapendekezo ya Nambari ya Huduma yalipingwa katika Mahakama ya Juu ya Kenya na mashirika ya haki za binadamu kwa sababu, zikiwemo zingine, hitaji la kushirikishwa kwa umma na tetesi kuwa mapendekezo yalilenga kuyanyima haki makundi ambayo tayari yalikuwa yametengwa nchini kama vile watu wasio na uraia. Jambo moja lililozua tetesi zaidi ni kwenye mradi huu wa serikali kiuhakika ni kuwa usajili wa Nambari ya Huduma ulikuwa ni wa lazima ili kuweza kupokea huduma za serikali kama vile matibabu. Mahakama ya juu ilitoa maamuzi kwamba hatua hii ya serikali ilikuwa ya kikatiba mradi tu taarifa zingelindwa vilivyo. Mahakama pia ilionelea kuwa ukusanyaji wowote wa vinasaba (DNA) na kurekodi kwa eneo halisi la mtu ilikuwa ya kuingilia na isiyo ya kikatiba kwani ilikuwa ukiukaji wa faragha yao.[5] Upande wa mashtaka haukukubaliana na vipengele fulani vya uamuzi wa Mahakama ya juu kuhusu jambo hili na uliwasilisha rufaa katika Mahakama ya Rufaa. Rufaa hii bado haijasikilizwa na kuamuliwa kikamilifu.

Cha msingi, Muswada wa Nambari ya Huduma hauna vifungu vya kutosha kuhusu hatua za ulindaji data. Kuanzishwa kwa sajili kuu ya umma kushiriki data na mashirika anuai ya serikali na / au hifadhi data za kibinafsi na watumiaji kwa huduma anuwai na shughuli zinaleta hatari kwa faragha ambayo ni tofauti kabisa na hali iliyopo pale ambapo data inahifadhiwa katika hifadhidata tofauti. Muswada unapendekeza hatua mbali mbali za adhabu kwa kutofuata masharti anuwai ya Muswada.[6] Matumaini ni kwamba nambari ya Huduma itatekelezwa kwa kufuata masharti makali kama ilivyoamuliwa na Mahakama ya juu katika kesi hiyo ili kulinda data za kibinafsi za umma.

MATAMSHI YA CHUKI, TAARIFA POTOFU NA SHERIA ZA MAKOSA YA JINAI

Sheria ya matumizi mabaya ya kompyuta na Uhalifu wa ki-mtandao[7]

Mnamo Julai 2019, Bunge la Seneti lilienda Mahakama ya juu kupinga uhalali wa sheria 24 zilizokuwa zimepitishwa na Bunge la Kitaifa bila kulishirikisha Bunge hilo la Seneti, mojawapo wa vyumba vya Bunge. Kenya ni nchi yenye Bunge mbili. Baada ya kusikiliza na kubaini mashtaka, Mahakama ya juu ilibatili idadi ya Miswada ambayo ilipitishwa na Bunge la Kitaifa ambayo haikuhusisha Seneti. Sheria ambazo zilifutwa ni pamoja na Sheria ya Matumizi Mabaya ya Kompyuta na Sheria ya Makosa ya Mtandaoni, sheria kuu ya TEHAMA nchini Kenya. Mahakama ya juu ilisitisha uamuzi wao kwa muda wa miezi tisa ili kulipa bunge muda wa kutosha wa kurekebisha makosa kama inavyobainiwa na Mahakama. Bunge la Kitaifa limetishia kuwasilisha rufaa dhidi ya uamuzi huu. Maana ya uamuzi wa Mahakama ya juu ni kwamba sheria hizo zitakoma kutumika baada ya miezi tisa, kwa kufuata agizo la Mahakama.

5. Huduma Namba: Kenya court halts biometric ID over data fears: https://www.bbc.com/news/world-africa-51324954
6. Seven Things You Should Know About Huduma Number, https://icj-kenya.org/news/latest-news/271-seven-things-you-should-know-about-huduma-namba
7. High Court nullifies 23 laws passed without Senate's approval, https://www.businessdailyafrica.com/bd/news/high-court-nullifies-24-laws-senate-s-approval-2725652



Kenya ilipiga hatua chanya katika haki za kidijitali na ujumuishaji wa kidijitali mnamo mwaka wa 2020.

KUTENGWA KIDIJITALI

JINSIA NA TEHAMA

Wanawake wengi nchini Kenya hawafikii huduma ya simu za rununu na wengine wanamiliki SIM kadi tu ambayo inamaanisha kuwa wanategemea marafiki na majirani kupata huduma za simu. Ni muhimu kuelewa changamoto ambazo wanawake wanakabiliwa nazo katika ufikiaji rasilimali za kidijitali. Changamoto kuu tatu ambazo mara nyingi hutambuliwa ni pamoja na kumudu, umuhimu na ukosefu wa ujuzi wa kidijitali kati ya wahusika wa jinsia fulani. Miundombinu ya kidijitali ya nchi haipo imara sana na kuna mgawanyiko wa vijijini-mijini na vile vile kutengwa kidijitali kwa jinsia katika sehemu za nchi haswa Kaskazini.

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

- Serikali inapaswa kushughulikia swala la ukosefu wa usawa wa ujumuishwaji kidijitali wakati huu na hata baada ya kipindi cha janga la CIVID-19
- Serikali inapaswa kushughulikia pengo la usawa wa kijinsia ili kuhakikisha kuwa wanaume na wanawake na vijana pia wana fikiwa na mtandao bila vizuizi.
- Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa utoaji wa nambari ya Huduma uliopangwa haukiuki haki za binadamu na utekelezaji wake unalingana na uamuzi wa mahakama katika kesi ya Nambari ya Huduma.

Utafiti Maalum: Tishio kwa faragha ya data Kenya wakati wa COVID-19

Imeandaliwa na Ekai Nabenyo

Ingawa janga la COVID-19 ni la ulimwengu, ukuzaji na utekelezaji wa ufuatiliaji wa mawasiliano umefanyika tu katika ngazi za kitaifa. Mwanzoni mwa janga la COVID-19, njia tofauti zilitumiwa na serikali ya Kenya kuzuia kuenea kwa janga hilo. Hii ilijumuisha agizo la lazima la karantini kwa watu wote wanaosafiri kwenda Kenya. Chali Baluu (jina limebadilishwa), raia wa Kenya, aliripoti ukiukwaji wa haki za binadamu kwa Tume ya Haki za Binadamu ya Kenya, akilalamika kuwa vifaa vyake vya mawasiliano, haswa simu zake za rununu, vilifuatiliwa na mamlaka za serikali. Matukio mengi pia yaliripotiwa kuhusu kuingiliwa na kusikizwa mawasiliano ya kibinafsi. Kwa kuongezea, kama mgonjwa wa COVID-19, Chali Balu aliiambia Tume ya Haki za Binadamu ya Kenya (KHRC) kwamba wakati walipowekwa karantini kwa lazima katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta jijini Nairobi, kwa kufuata agizo la serikali, waliwekwa chini ya uangalizi wa masaa 24/7.

Changamoto iliyokabiliwa na KHRC katika kufuatilia ukweli au vinginevyo vya ukiukwaji huu ni pamoja na ukweli kwamba haikuwa rahisi kudhibitisha ufuatiliaji wa vifaa vya mawasiliano licha ya uzito wa madai yaliyotolewa. Watu waliripoti matukio kwa KHRC ambayo waliwekwa chini ya lazima kwa karantini kwa vipindi zaidi ya siku 14 zilizotajwa. Hii ilimaanisha ufuatiliaji zaidi kwa vipindi virefu au visivyojulikana. Kwa kuongezea, ukweli kwamba wafanyikazi wa KHRC walifanya kazi karibu ilimaanisha kwamba walipokea na kushughulikia ripoti hizi za ukiukwaji kwa karibu zaidi. Hii iliathiri uaminifu ambao ni rahisi kudhibitisha wakati wa mawasiliano ya ana kwa ana. Inamaanisha pia kwamba visa kadhaa vya wale wahasiriwa wa teknolojia ambao wangeweza kutembelea ofisi za Tume wanaweza kuwa hawajaripotiwa. Waandishi wa habari ambao walijaribu kupeleka habari za ukiukwaji wa haki za binadamu wa COVID-19 kwa umma kwa jumla walikamatwa wakati ufuatiliaji uliongezwa kwenye ofisi za vyombo vya habari, na uharibifu mkubwa uliripotiwa. Baraza la Habari la Kenya liliwasilisha malalamiko dhidi ya ukiukwaji huu ambao kimsingi ulikiuka haki ya kupata habari iliyohakikishiwa chini ya Katiba ya Kenya, 2010. Kifungu cha 35 (1) cha Katiba ya Kenya kinasema kama ifuatavyo:

Kila raia ana haki ya kupata -

(a) habari inayoshikiliwa na Serikali; na

(b) habari inayoshikiliwa na mtu mwingine na inayohitajika kwa utekelezaji au ulinzi wa haki yoyote au uhuru wa kimsingi.

(c) Kila mtu ana haki ya kusahihishwa au kufutwa kwa habari isiyo ya kweli au ya kupotosha inayoathiri mtu huyo.

(d) Serikali itachapisha na kutangaza habari yoyote muhimu inayoathiri taifa.

Vyombo vya haki za binadamu vya kikanda na kimataifa kama vile Azimio la Kanuni za Uhuru wa Kujieleza na Ufikiaji wa Habari barani Afrika vinadai kwamba kwa kizuizi chochote kwa upatikanaji wa habari inayoshikiliwa na mamlaka za umma kuruhusiwa na sheria, lazima iwe na lengo halali, lazima , sawia na lengo la kulinda afya ya umma, na lazima pia iwekewe tu kwa uwepo wakati wa majanga. Hii inamaanisha kwamba mapungufu yoyote ya haki za binadamu yanapaswa kuhesabiwa haki. Ufikiaji wa habari ni sehemu muhimu ya haki ya afya na nchi kama Kenya zinahimizwa kufuata. Wakati maafisa hawatachapisha habari za kiafya kama inavyotakiwa, idadi ya watu hupata athari mbaya za kiafya na hawawezi kufurahia haki yao ya afya kama ilivyohakikishiwa. Kenya inahitaji wazi, kuwa na usikivu na uwajibikaji kwa raia katika vita dhidi ya COVID-19.

Kupunguzwa kwa haki ya umma ya kufahamu shughuli za serikali zao ni kinyume na tija kwa juhudi katika kupambana na mlipuko wa COVID-19. Haki ya kupata habari ni muhimu kwa kuhakikisha ufahamu na uaminifu wa umma, kupambana na habari potofu, kuhakikisha uwajibikaji na pia kuendeleza na kufuatilia utekelezaji wa sera za umma zinazolenga kukabiliana na majanga. Ni muhimu kwamba haki ya kupata habari itunzwe wakati wa dharura kadri inavyowezekana.

Utafiti maalum: Wakenya wanaolinda usalama wa Data wakati wa janga

Imeandaliwa na Ekai Nabenyo

Ufuatiliaji wa maambukizi, kama mchakato wa usimamizi wa afya ya umma wa kutambua watu (pamoja na wafanyakazi wa huduma ya afya) ambao watakuwa wamepata maambukizo ya COVID-19 yaaliyo dhibitishwa, ili tumika Kenya, kama ilivyo katika nchi zingine. Ufuatiliaji wa maambukizi unamaanisha kutambua kesi za mara ya pili zinazoweza kutokea kutoka kwa kesi ya awali ya COVID-19. Uingiliaji huu umesaidia kuzuia maambukizi zaidi na wahasiriwa. Utekelezaji wa ufuatiliaji wa maambukizi nchini Kenya na Wizara ya Afya, kwa uratibu na utekelezaji wa sheria, haujawa na utata na imeibua wasiwasi mwingi wa haki za binadamu. Mambo muhimu ni pamoja na ufanisi wa utafatiliaji wa maambukizi na athari zinayofanana hasa faragha na haki za binadamu. Kusuasua kwa ufuatiliaji wa maambukizi huenda zaidi ya kuzingatia faragha na uwezekano wa kukiuka haki zingine za kibinadamu. Ingawa baadhi ya akaunti kama walivyoeleza na wahojiwa ni za kweli, majina ambayo yametumika katika utafiti huu yamebadilishwa kwa makusudi ili kuficha utambulisho wa kweli wa wahojiwa.

Mwandishi wa habari wa The Standard Media Group alipokea ripoti kutoka kwa Wanjiru Kemboi ambaye simu zake na mawasiliano mengine yalidhaniwa kuingiliwa kijasusi na wakala wa ufuatiliaji wa serikali. Ilionekana pia kuwa watu walioathiriwa hawakuelewa haki zao za kidijitali. Wanjiru ambaye alikuwa amekabiliwa na kipindi cha lazima cha kukaa karantini kwa siku 14 aliwasiliana na mwandishi wa habari kwani alikuwa na tuhuma nzito kwamba simu zake za rununu zinafatiliwa, ingawa alionekana kutokuwa na wasiwasi nayo. Wanjiru alikuwa na uzoefu ambapo afisa wa Huduma ya Upelelezi wa Kitaifa aliwasiliana naye, kama mgonjwa ambaye alipaswa kujitenga, akimwonya Wanjiru dhidi ya kwenda sokoni na kuchangamana na wengine siku ambayo alijaribu kwenda sokoni. Wanjiru Kemboi alitii agizo hilo na kurudi tena kwa karantini. Huu ulikuwa ushuhuda wazi kwamba mgonjwa alikuwa akifuatiliwa na Idara yaa Kitaifa ya Ujasusi kwa kushirikiana na Idara ya Ufuatiliaji wa Afya. Hii ilimaanisha kuwa mgonjwa wa COVID-19 aliishi kwa hofu kila wakati akiwa kifungoni na hakuwa na uhakika wa ulinzi wa faragha zake. Haikujulikana pia ni kiwango gani cha ufuatiliaji wa ufuatiliaji na upenyeshaji wa Idara ya Kitaifa ya Ujasusi, na Ufuatiliaji wa Afya.

Hii ni wazi ilikiuka haki ya mtu ya faragha, hata katika janga la COVID-19, kama ilivyohakikishiwa katika Muswada wa Haki za Katiba ya Kenya, 2010. Ufunuo huu unazua maswali kuhusu jinsi data ya mgonjwa wa COVID-19 inatumiwa na inapaswa kuhifadhiwa kwa muda gani kwenye hifadhidata za usalama wa taifa. Wasiwasi hapa ni uwezekano wa ufuatiliaji na Serikali, haswa ikiwa matumizi na uhifadhi wa data hautalindwa kisheria. Haki ya kibinafsi ya faragha inaweza kuathiriwa na ukusanyaji na data ya kidijitali. Katika kuandaa suluhisho la kushughulikia majanga, taasisi za serikali na wasimamizi wanapaswa kufanya kila wawezalo kusawazisha haki ya faragha na haki ya habari wakati kuna uwezekano wa mgogoro kati yao. Kesi nyingine nyingi ziliripotiwa, haswa baada ya mwandishi wa habari kuandika nakala ili kuripoti visa vya kuongezeka kupigiwa simu na mashirika ya Serikali.

Kwa kumalizia, kufatilia maambukizi imezua mabaya ambayo yanakiuka haki za binadamu husababisha hali ya sintofahamu kati ya Serikali na raia. Ili kurekebisha makosa ambayo yanaonyesha ufuatiliaji wa maambukizi nchini Kenya, inashauriwa kuwa kuna haja ya haraka kwa mamlaka ya Ufuatiliaji wa Afya na maafisa wa Usalama wa Taifa ya Ujasusi kufuata masharti ya Sheria ya Ulinzi wa Takwimu, 2019, hadi ulinzi wa data za kibinafsi ya raia. Serikali inapaswa kuchukua hatua madhubuti kulinda data na kudhibiti ni nani mwenye kuzifikia data hizo.

Serikali ya Kenya ilianzisha programu ya mSafiri, ya wazo la ushirikiano kati ya Wizara ya Afya ya Kenya na Wizara ya Uchukuzi, katika kufuatilia kuenea kwa virusi. Programu hiyo iliundwa kutoa data muhimu ambazo itasaidia kufatilia kesi za awali zilizoambukizwa au zinazoshukiwa za COVID-19. Chombo hiki cha Ufuatiliaji wa Afya ya Kidijitali kilihitaji uhakikisho wa serikali kuwa wazi jinsi data iliyokusanywa ilitumika lakini ukosefu wa kanuni elekezi, kulingana na ufuatiliaji wa maambukizi kwa njia ya mawasiliano, ilikuwa jambo lenye hofu lililoibuliwa. Kulikuwa na wasiwasi na wagonjwa fulani kwamba Serikali ya Kenya haikuweza kusimamia teknolojia hizi na kwa hivyo ilishirikiana na kampuni za tatu za teknolojia. Kama matokeo, hii imewasilisha fursa ya matumizi mabaya ya data ya ufuatiliaji wa afya kwani hakuna Mikataba ya ushirikiano wa Kitakwimu inayojulikana na watu wengine. Hii ni muhimu kwani inahofiwa kuwa utumiaji data wa serikali nchini Kenya unaweza kutumiwa zaidi kwa sababu za kiusalama; kuna haja ya kulinda data dhidi ya hatua hiyo.

LONDA

KENYA HAKI ZA DIGITALI NA UJUMUISHAJI 2020 RIPOTI

UCHAPISHAJI WA PARADIGM INITIATIVE

PARADIGM INITIATIVE

Paradigm Initiative
374 Borno Way, Yaba, Lagos, Nigeria
Email: media@paradigmhq.org
www.paradigmhq.org
@ParadigmHQ